TAARIFA YA KUONGEZA USHIRIKI WA WASICHANA KATIKA KUCHUKUA NA KUTUMIA MIKOPO YENYE MASHARTI NAFUU / ISIYO NA RIBA ITOLEWAYO NA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA, 2019 – 2021.

1.0 Utangulizi

Halmashauri zote nchini zinapaswa kutenga na kutoa mikopo ya asilimia 10 ya makusanyo yake ya ndani kwa makundi ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kwa uwiano wa asilimia 4, 4 na 2 mtawalia.

Kwa bahati mbaya, utaratibu wa mikopo ya vijana (4%) imekuwa ikinufaisha kundi moja tu, la vijana wa kiume katika jamii ya Shinyanga Manispaa. Ushiriki wa vijana wakike (wasichana) katika kuchukua na kutumia mikopo kwa kundi hili ni mdogo ukilinganisha na wenzao vijana wa kiume.

2.0 Mkakati wa Mabadiliko

Kwaujumla, mkakati wa kuongeza ushiriki wa wasichana kwenye mikopo hii ya asilimia 4 ni pamoja na kuongeza uelewa wa masuala ya jinsia na kubadili au kuboresha mfumo wa utoaji wa mikopo (4%) kwa kuzingatia jinsi. Shughuli hizi zitategemea kujumuisha usawa wa kijinsia katika utoaji wa mikopo ambapo makundi yote yafikiriwe kwa usawa ili wote wanufaike.

Katika kufikia lengo hili shughuli zifuatazo zilipangwa kufanyika;-

1. Kujenga uelewa kwa wasichana 340 wanaomaliza (waliopo shuleni) juu ya uwepo wa mikopo hii na namna ya kuweza kuifikia.
2. Kuwajengea uwezo vijana wa kike 1,560 walio nje ya mfumo wa elimu (waliomaliza shule) juu ya elimu ya kujitambua, kubuni na kusimamia biashara, na uwepo wa mikopo ya asilimia 4 itolewayo na Halmashauri.
3. Kuanzisha na kulea kikundi kimoja cha wasichana cha mfano. Kitakacho jengewa uwezo na kupewa mkopo ili kuendesha shughuli za kiuchumi.
4. Kujenga uelewa kwa viongozi na watendaji juu ya mapungufu yaliyopo katika utoaji wa mikopo kwa vijana (4%) kwa kuzingatia jinsi.

3.0 Hali ya Utekelezaji

a) Kikao cha kuwajengea uwezo maafisa maendeleo ya jamii ngazi ya kata kilifanyika 30/02/2020 ambapo maafisa kutoka kata zote 17 walishiriki. Lengo likiwa ni kubainisha mapungufu yaliyopo katika utoaji wa mikopo ya asilimia 4 kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na kujadiliana namna bora ya kuongeza ushiriki wa vijana wa kike katika kuchukua na kutumia mikopo hii.

b) Kikao cha siku moja 03/03/2020 kilifanyika kwa ufadhili wa CRDB Bank katika Ukumbi wa Kalinjuna. Kikao kilihusisha vijana 36 (28 vijana wa kike na 8 vijana wa kiume) walio nje ya mfumo wa shule kutoka katika kata za Ndembezi, Ngokolo na Mjini. Lengo likiwa ni kuwajengea uwezo vijana walio nje ya mfumo wa elimu juu ya kujitambua, kubuni, kuanzisha na kusimamia biashara, na

uwepo wa mikopo ya asilimia 4 pamoja na mikopo itolewayo na taasisi za benki (CRDB). Mada zilizowasilishwa ni; Kujenga uwezo wa kiuchumi kwa wanawake na vijana kupitia ushiriki katika kazi za mikono, ufugaji na viwanda vidogovidogo, Utoaji wa mikopo nafuu ya asilimia 4 ya Halmashauri ya Manispaa na mikopo kutoka CRDB na Kujiunga na bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF).

c) Mafunzo ya kujenga uelewa juu ya stadi za maisha, kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI, Kujiunga na huduma ya bima ya afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) na kujenga uwezo wa kiuchumi kupitia fursa ya mikopo ya asilimia 4 itolewayo na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Jumla ya wasichana 400 na wavulana 100 kutoka katika chuo cha VETA Shinyanga na chuo cha Biashara (MUCCOBS) tawi la Shinyanga wamefikiwa. Mafunzo yaliendeshwa tarehe 6 na 12 Machi, 2020 chuo cha VETA na MUCCOBS mtawalia.

d) Tumeweza kuwafikia viongozi wa kamati za maendeleo za kata na maafisa ugani kutoka katika kata 3 za Ndembezi, Mjini na Chamaguha kupitia vikao vya WDC katika kata husika. Lengo likiwa ni kuwajenga uelewa viongozi na watendaji juu ya mapungufu yaliyopo katika utoaji wa mikopo ya asilimia 4 kwa vijana kwa kuzingatia jinsi na kuwataka kuhamasisha vijana wa kike katika maeneo yao kujitokeza, kuchukua na kutumia mikopo hii nafuu itolewayo na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

e) Vipindi viwili (2) vya redio vimefanyika tarehe 09/09/2020 na 21/04/2021 katika kituo cha redio faraja kilichopo Manispaa ambapo mada zilikua uwezeshaji wa vijana wakike kiuchumi kupitia fursa ya mikopo ya asilimia 4 inayotolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga pamoja na kuzuia na kupambana na vitendo vya kikatili dhidi ya watoto na wanawake.

f) Kutembelea vikundi kumi (10) vya wasichana vilivyopo kwenye mradi wa ***Dream*** ili kuona shughuli zao na kuwajengea uwezo katika kujiwezesha kiuchumi ikiwemo kutumia fursa ya mikopo nafuu itolewayo na Halmashauri ya Manispaa Shinyanga, Kuwaelekeza taratibu za usajili wa vikundi na Masuala ya ukatili wa kijinsia pamoja na kuwapa Mafunzo kuhusu kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI. Vikundi hivi vina jumla ya vijana wakike 180 ambapo kila kikundi kina wanachama 18. Vikundi vilivyotembelewa ni vya kata 7 za;- Kolandoto (*Vikundi vya Kipepeo one na Kipepeo two)*, Ndala (*Kikundi cha* Shujaa), Ibadakuli (*Vikundi vya Tumaini, Uwazi na Tutashinda*), Kitangili (*Kikundi cha Ushirika*), Ibinzamata (*Kikundi cha Malaika*), Chibe (*Kikundi cha Mawasiliano*) na Old Shinyanga (*Kikundi cha Chemshabongo*) wanaojishughulisha na biashara ndogondogo pamoja na shughuli za kuweka na kukopa. Aidha, kuna vikundi zaidi ya 244 katika kata zote 17 za Halmashauri ambavyo vimeundwa na kujengewa

uwezo kwa ushirikiano wa timu ya Maafisa wa Halmashauri ya Manispaa na asasi za Rafiki SDO na Restless.

g) Kulea vikundi viwili (2) kwa ajili ya kupata vikundi vya mfano. Kikundi kimojawapo ni ***Nguvu ya Msichana*** cha Old Shinyanga ambacho kimepatiwa mafunzo na SIDO juu ya utengenezaji wa vitafunwa kupitia Mradi wa ***Vijana Tunaweza*** unaoendeshwa na Shirika la Restless. Kikundi kingine kinatarajiwa kuwa ni miongoni mwa vikundi vilivyoanzishwa kupitia mradi wa ***Dream*** unaofadhiliwa na Shirika la Rafiki SDO. Idara ya Maendeleo ya Jamii imewajengea uwezo vikundi vyote hivyo katika kujiwezesha kiuchumi ikiwemo kutumia fursa ya mikopo nafuu (asilimia 4) itolewayo na Halmashauri ya Manispaa Shinyanga

4. Changamoto

i. Kukosekana kwa kikundi/vikundi vya mfano vya vijana wa kike na watu wenye ulemavu vitakavyohamasisha wenzao kujitokeza katika kuchukua na kutumia mikopo ya asilimia 4 na asilimia 2.

ii. Uelewa na muitikio mdogo kwa vijana hasa wakike katika kujitokeza kwenye shughuli mbalimbali zenye kuibua fursa kwa makundi hayo, *mfano kikao cha vijana cha tarehe 03/03/2020 kilitarajiwa kupokea vijana 100 lakini waliofika na kushiriki ni vijana 36 tu*.

iii. Utoaji wa mikopo kwa vijana haujazingatia usawa kijinsia hali inayopelekea vijana wa kiume kuendelea kunufaika zaidi ya wenzao vijana wa kike.

5.0 Mapendekezo

i. Maofisa maendeleo ya Jamii ngazi ya kata walipendekeza kuwepo na vikundi viwili vya kulelewa kikiwemo kikundi kimoja kitakachohusisha wasichana wenye ulemavu ili nao waweze kutoa mfano kwa watu wa kundi hilo.

ii. Kuendelea kujenga uelewa kwa makundi tofauti juu ya kuongeza ushiriki wa wasichana katika kuchukua na kutumia mikopo yenye masharti nafuu (asilimia 4%), hii ni pamoja na kuongeza ushiriki wa wasichana katika kundi la watu wenye ulemavu (asilimia 2%)

iii. Vikundi vya vijana wa kike (wasichana) vilivyojengewa uwezo vipatiwe mikopo ili kuviwezesha kujikwamua kiuchumi sambamba na kuvunja/kuondoa dhana ya mapungufu yaliyopo katika utoaji wa mikopo kwa kuzingatia jinsi. Aidha, vikundi viwili vya mfano vilivyoandaliwa vipatiwe mikopo ili kuweza kutoa mifano hai kwa jamii na kuongeza ushiriki wa wasichana katika kuchukua na kutumia mikopo ya asilimia 4% kwa vijana na asilimia 2% kwa kundi la watu wenye ulemavu.